policy forum

MWONGOZO WA UANACHAMA WA POLICY FORUM 2022

KUHUSU POLICY FORUM

Policy Forum (PF) ni mtandao wa mashirika yasiyo ya kiserikali (NGO) yapatayo 60 ulionzishwa mwaka 2003 na kusajiliwa chini Sheria ya Mashirika yasiyo ya kiserikali ya mwaka 2002 ikiwa na usajili namba NGO/R2/00015. Policy Forum ina wanachama mbalimbali ambao hujumuika kwa pamoja wakiwa na malengo ya kushawishi michakato ya kisera ili kupunguza umasikini, kuongeza usawa na demokrasia; huku mkazo mkubwa ukiwekwa katika uwajibikaji kwenye matumizi ya fedha za umma katika ngazi ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa. Mabadiliko yanayotarajiwa na Policy Forum ni maboresho ya utoaji huduma kwa kuzingatia utawala bora ulioimarishwa na uwajibikaji wa matumizi ya rasilimali za umma.

UANACHAMA

Uanachama wa Mtandao wa Policy Forum ni wa hiyari na upo wazi kwa shirikika lolote lisilo la kiserikali lililo sajiliwa Tanzania bara na ambalo malengo yake yanaendana na dira, dhima na malengo ya PF kama yanavyojieleza katika Mpango Mkakati wake.

FAIDA ZA UANACHAMA

Uanachama wa PF unaweza kufaidisha shirika lako kama ifuatavyo:

KUJENGEWA UWEZO

Mtandao wa PF hutoa mafunzo yanayohusu mada mbalimbali kwa wanachama wake kulingana na mahitaji ya wanachama. Pia, wanachama huongezewa maarifa kwa kupitia nyenzo kama vile majarida, taarifa na vipeperushi vinavyochambua sera mbalimbali ambavyo husambazwa kwa njia ya vifurushi.

UPATIKANAJI WA WATUNGA SERA/WAFANYA MAAMUZI

Mtandao wa PF hutoa nafasi kwa wanachama wake kufanya uchechemuzi kwa watunga sera na wafanya maamuzi kwa malengo ya kushawishi uwepo wa uwazi na uwajibikaji katika matumizi ya rasilimali za umma kwenye sekta mbalimbali ambazo wanachama wanafanyia kazi.

KUJUMUIKA KWENYE MITANDAO

Wanachama wa PF huweza kujiunga na mitandao mbalimbali ya kitaifa, ya watu binafsi na mashirika yenye dhima zinazoendana, hali hii hupelekea kupatikana kwa makundi yanayoshabihiana ambayo huweza kubadilishana taarifa, mawazo na ujuzi. Policy Forum huratibu warsha za kujifunza, midahalo ya kisera ya kila mwisho wa mwezi, ziara za kimataifa za kujifunza na mikutano ya kutafakari ya kikanda ambayo hutoa fursa ya uanzishwaji wa ubia na mashirika mengine yasiyo ya kiserikali.

KUJULIKANA

Tunatoa taarifa za kazi za wanachama kupitia tovuti yetu, mitandao ya kijamii na kwa washirika wa Kimataifa.

NGUVU YA KUFANYA MAAMUZI

Kila mwaka, wanachama hupitisha mpango kazi na bajeti ya mtandao pamoja na taarifa za kifedha na utekelezaji za mwaka uliopita. Pamoja na hayo, wanachama wana nguvu ya kupiga kura kuchagua wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi. Kupitia vikundi kazi, wanachama wana nguvu ya kuamua kazi ambazo zitapewa kipaumbele kwenye utekelezaji wa mwaka husika. Wanachama ndiyo huongoza katika utekelezaji wa kazi za mwaka huku jukumu la uratibu likifanywa na sekretarieti.

UTAFUTAJI FEDHA WA PAMOJA

Tunajumuika na wanachama kwenye utafutaji wa fedha za kutekeleza kazi zinazoshabihiana. Pia mtandao hutoa taarifa za nafasi mbalimbali za upatikanaji wa fedha za kufanyia kazi kupitia taarifa za kila wiki. Pia, wanachama hupatiwa mafunzo ya kuwajengea uwezo wa kutafuta fedha na mbinu za kushinda nafasi hizo zinapotangazwa.

FURSA YA KUSHIRIKI MATUKIO YA KITAIFA NA KIMATAIFA

Policy Forum kama mtandao hushiriki katika matukio tofauti ya kitaifa na kimataifa ambayo yanalenga kushawishi michakato ya sera yenye mrengo wa kuboresha usimamizi bora wa rasilimali za umma. Kupitia matukio haya wanachama wa Policy Forum huweza kufikia watoa maamuzi wa kitaifa na kimataifa hivyo kupata fursa ya kushawishi mabadiliko ya sera.

KUNUFAIKA NA UBIA ULIOPO BAINA YA POLICY FORUM NA SERIKALI

Mtandao wa Policy Forum ina ushirikiano rasmi na wizara na taasisi mbalimbali za serikali kupitia mikataba ya makubalino (MoU). PF imesaini Mikataba wa Makubaliano na Ofisi ya Rais-Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) na Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB). Kutokana na ushirikiano hasa na TAMISEMI, wanachama wa PF huweza kupata urahisi wa kutenda kazi za ushawishi wa sera katika ngazi ya msingi na kitaifa.

USHAWISHI WA SERA WA PAMOJA

Kwa miaka mingi PF kwa njia za kimkakati imekuwa ikitoa nafasi kwa wanachama wake kufanya uchechemuzi kushawishi mabadiliko ya sera ili kuimarisha matumizi sahihi ya rasilimali za umma. Wanachama wa mtandao kupitia vikundi kazi huongoza katika utekelezaji wa kazi kama ilivyoainishwa katika mipango. Mbinu zetu za pamoja zinazotumia uchechemuzi unaozingatia ushahidi huongeza thamani katika juhudi za mabadiliko ya sera na michakato inayodhamiria kuboresha maisha ya Watanzania.

WAJIBU WA WANACHAMA

I. Kuchagua/kupiga kura, kuchaguliwa/kupigiwa kura kuwa katika uongozi wa Shirika;
II. Kuhudhuria Mkutano Mkuu;
III. Kushiriki katika shughuli zote za Shirika kadiri itakavyohitajika kufanya hivyo;
IV. Kupokea taarifa za maendeleo ya Shirika kwa njia yoyote ya mawasiliano;
V. Kulipa ada zilizoainishwa na Mkutano Mkuu;
VI. Kuhudhuria mikutano yote inayohitaji uwepo wao;
VII. Kutunza siri za mambo na maamuzi yote ya Shirika.

NANI ANAWEZA KUWA MWANACHAMA?

Tunakaribisha maombi ya mashirika yasiyo ya kiserikali ambayo:

I. Mashirika yasiyo ya kiserikali yenye angalau miaka miwili ya ufanyaji kazi uchechemuzi wa kushawishi utawala bora na uwajibikaji wa matumizi ya rasilimali za umma
II. Kujitolea kushiriki kwenye kazi za PF kama zilivyoainishwa kwenye Mpango Mkakati
III. Kuendana na dira, dhima na maadili yetu
IV. Kuheshimu utofauti wa kitamaduni, kupinga aina zote za ubaguzi na kutofungamana na upande wowote (kutohusika au kupendelea mgombeaji wa kisiasa au chama)

UPO TAYARI KUJIUNGA NASI?
TUMA MAOMBI KUPITIA

www.policyforum-tz.org/sw/members

policy forum

Mtaa wa Ndovu, Barabara ya Rose Garden
Nyumba Namba 7
S.L.P 38486, Dar es Salaam
Simu: +255 22 2780200
Simu: +255 782 317434
Barua Pepe: info@policyforum.or.tz
Tovuti: www.policyforum.or.tz